# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA HAMSINI NA NNE

**26 JUNI, 2025**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

### KIKAO CHA HAMSINI NA NNE - TAREHE 26 JUNI, 2025

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):**

Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

**WAZIRI WA FEDHA:**

Maelezo ya Waziri wa Fedha kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Shirika la Fedha la Afrika *(Agreement for the Establishment of the Africa Finance Corporation – AFC).*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

Maelezo ya Waziri wa Maliasili na Utalii kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Marekebisho ya Mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Shirika la Fedha la Afrika *(Agreement for the Establishment of the Africa Finance Corporation – AFC).*

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Marekebisho ya Mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere.

## III. MASWALI:

## OFISI YA WAZIRI MKUU:

**690 MHESHIMIWA MARIAM NASSORO KISANGI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha majengo ya Mradi wa Dege Beach – NSSF Mbweni kwa kuwa ni wa muda mrefu.

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**691 MHESHIMIWA JOSEPH GEORGE KAKUNDA (SIKONGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Zahanati za Molemlimani, Muungano, Isanjandugu, Urafiki, Iyombakuzova na Kapumpa zitakamilika.

**692 MHESHIMIWA JACQUELINE KAINJA ANDREW (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini TARURA itaweza kutengeneza Barabara zenye viwango zisizoharibika kipindi cha mvua.

**693 MHESHIMIWA JACKSON GEDION KISWAGA (KALENGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Bweni la Wasichana na Wavulana katika Shule ya Sekondari ya Kimaiga Kata ya Kihanga.

**694 MHESHIMIWA TARIMBA GULAM ABBAS (KINONDONI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali haioni haja kutafuta fedha kama mikopo kuliko kutegemea Bajeti ya Serikali kuweka Lami, Taa na Mifereji Barabara za ndani Dar es Salaam.

**WIZARA YA UJENZI:**

**695 MHESHIMIWA DKT. CHRISTINA CHRISTOPHER MNZAVA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuunganisha Barabara kutoka Nyamilangano - Ushetu hadi Kaliua Tabora.

**696 MHESHIMIWA JOSEPHAT SINKAMBA KANDEGE (KALAMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, Iini Serikali itaanza ujenzi wa kiwango cha lami Barabara kutoka Mji Mdogo wa Laela – Mwimbi hadi Matai kuunganisha na Barabara ya Kasanga.

**WIZARA YA AFYA:**

**697 MHESHIMIWA KABULA ENOCK SHITOBELA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, lini Serikali itaongeza Wataalam wa Afya katika Hospitali ya Bugando na Sekou Toure kwa kuwa kuna upungufu mkubwa.

**IV. HOJA ZA SERIKALI:**

**MAAZIMIO:**

**WAZIRI WA FEDHA:**

Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Shirika la Fedha la Afrika *(Agreement for the Establishment of the Africa Finance Corporation – AFC).*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

Azimio la Bunge la Kuridhia Marekebisho ya Mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere.

**V. TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE:**

## VI. HOTUBA YA KUKAMILIKA KWA SHUGHULI ZA MKUTANO WA KUMI NA TISA WA BUNGE:

**WAZIRI MKUU:**

**DODOMA** 
**26 JUNI, 2025**

**BARAKA I. LEONARD** 
**KATIBU WA BUNGE**

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA